

**KUMB: PPR/16 - 02/1**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA  
JUMATANO, TAREHE 3 FEBRUARI 2016**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 3 Febuari 2016** Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 6 Januari 2016. Kwa Mwezi Februari 2016, bei ya reja reja ya mafuta ya Petroli na Dizeli zimeshuka kwa Sh 55/lita sawa na asilimia **2.91 na kwa Sh 147/lita sawa na asilimia 8.40** sawia, bei ya reja reja ya Mafuta ya Taa haijabadilika. Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita bei ya jumla kwa mafuta ya Petroli na Dizeli zimeshuka kwa Sh 55.27/lita sawa na asilimia 3.08 na kwa Sh **146.78/lita sawa na asilimia 8.94** sawia, aidha, bei ya jumla ya Mafuta ya Taa haijabadilika. Kuendelea kupungua kwa bei za mafuta kwenye soko la ndani kwa kiasi kikubwa kumetokana na kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia, na pia kushuka kwa gharama za usafarishaji/uletaji wa bidhaa za mafuta hayo kuja nchini. Hakukuwa na mafuta ya taa yaliyoingizwa nchini katika Mwezi Januari 2016, hivyo katika mwezi Februari 2016 bei ya bidhaa hii itaendelea kuwa kama ilivyokuwa kwa mwezi Januari 2016.
- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na *fomula* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye **Gazeti la Serikali Na. 405/2015 la Mwezi Julai 2015**.
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (e) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

## A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/lita)	Mafuta Ya Taa (Sh/Lita)
<b>Dar es Salaam</b>	1,842	1,600	1,699
<b>Arusha</b>	1,926	1,684	1,783
Arumeru (Usa West)	1,926	1,684	1,783
Karatu	1,945	1,702	1,801
Monduli	1,932	1,689	1,788
Ngorongoro (Loliondo)	1,983	1,740	1,839
<b>Kibaha</b>	1,847	1,604	1,704
Bagamoyo	1,853	1,611	1,710
Kisarawe	1,850	1,607	1,706
Mkuranga	1,852	1,610	1,709
Rufiji	1,870	1,627	1,727
<b>Dodoma</b>	1,901	1,658	1,758
Bahi	1,908	1,666	1,765
Chemba	1,927	1,685	1,784
Konooa	1,934	1,691	1,790
Kongwa	1,898	1,656	1,755
Mpwapwa	1,902	1,660	1,759
<b>Iringa</b>	1,906	1,664	1,763
Kilolo	1,911	1,668	1,767
Mufindi (Mafinga)	1,916	1,674	1,773
<b>Njombe</b>	1,934	1,692	1,791
Ludewa	1,972	1,730	1,829
Makete	1,965	1,723	1,822
Wanging'ombe (Igwachanya)	1,932	1,690	1,789
<b>Bukoba</b>	2,057	1,815	1,914
Biharamulo	2,032	1,789	1,888
Karagwe (Kayanga)	2,074	1,831	1,930
Kyerwa (Ruberwa)	2,079	1,837	1,936
Muleba	2,057	1,815	1,914
Ngara	2,023	1,780	1,879
Misenyi	2,066	1,823	1,922
<b>Geita</b>	2,007	1,765	1,864
Bukombe	1,996	1,754	1,853

Chato	2,028	1,786	1,885
Mbogwe	2,045	1,803	1,902
Nyang'hwale	2,022	1,780	1,879
<b>Kigoma</b>	2,073	1,831	1,930
Uvinza (Lugufu)	2,085	1,843	1,942
Buhigwe	2,062	1,820	1,919
Kakonko	2,030	1,788	1,887
Kasulu	2,059	1,817	1,916
Kibondo	2,038	1,795	1,894
<b>Moshi</b>	1,916	1,673	1,773
Hai (Bomang'ombe)	1,919	1,677	1,776
Mwanga	1,909	1,667	1,766
Rombo (Mkuu)	1,937	1,694	1,794
Same	1,902	1,660	1,759
Siha (Sanya Juu)	1,922	1,680	1,779
<b>Lindi</b>	1,901	1,659	1,758
Kilwa Masoko	1,876	1,634	1,733
Liwale	1,922	1,680	1,779
Nachingwea	1,930	1,688	1,787
Ruangwa	1,928	1,686	1,785
<b>Babati</b>	1,964	1,722	1,821
Hanang (Katesh)	1,975	1,732	1,832
Kiteto (Kibaya)	1,975	1,733	1,832
Mbulu	1,977	1,735	1,834
Simanjiro (Orkasumet)	1,996	1,754	1,853
<b>Musoma</b>	2,020	1,778	1,877
Rorya (Ingirijuu)	2,029	1,787	1,886
Bunda	2,012	1,769	1,868
Butiama	2,017	1,775	1,874
Serengeti (Mugumu)	2,066	1,824	1,923
Tarime	2,032	1,789	1,888
<b>Mbeya</b>	1,949	1,707	1,806
Chunya	1,959	1,716	1,815
Ileje	1,962	1,720	1,819
Kyela	1,965	1,722	1,822
Mbarali (Rujewa)	1,933	1,691	1,790
Mbozi (Vwawa)	1,958	1,716	1,815
Momba (Chitete)	1,967	1,725	1,824
Rungwe (Tukuyu)	1,958	1,716	1,815
<b>Morogoro</b>	1,867	1,625	1,724
Mikumi	1,883	1,640	1,740
Kilombero (Ifakara)	1,905	1,663	1,762

Ulanga (Mahenge)	1,916	1,673	1,772
Kilosa	1,886	1,643	1,742
Gairo	1,886	1,643	1,742
Mvomero (Wami Sokoine)	1,878	1,635	1,734
Turian	1,892	1,650	1,749
<b>Mtwara</b>	1,915	1,672	1,771
Nanyumbu (Mangaka)	1,963	1,721	1,820
Masasi	1,940	1,698	1,797
Newala	1,947	1,704	1,803
Tandahimba	1,940	1,697	1,796
<b>Mwanza</b>	1,992	1,750	1,849
Kwimba	2,028	1,786	1,885
Magu	2,000	1,758	1,857
Misungwi	1,998	1,755	1,854
Sengerema	2,024	1,782	1,881
Ukerewe	2,051	1,809	1,908
<b>Sumbawanga</b>	2,015	1,772	1,872
Kalambo (Matai)	2,007	1,765	1,864
Nkasi (Namanye)	2,028	1,786	1,885
<b>Katavi (Mpanda)</b>	2,050	1,807	1,906
Mlele (Inyonga)	2,028	1,786	1,885
<b>Songea</b>	1,965	1,723	1,822
Mbinga	1,999	1,756	1,856
Namtumbo	1,995	1,752	1,851
Nyasa (Mbamba Bay)	2,001	1,759	1,858
Tunduru	2,024	1,782	1,881
<b>Shinyanga</b>	1,971	1,728	1,828
Kahama	1,985	1,742	1,841
Kishapu	1,999	1,757	1,856
<b>Simiyu (Bariadi)</b>	2,012	1,770	1,869
Busega (Nyashimo)	2,005	1,763	1,862
Itilima (Lagangabilili)	2,015	1,773	1,872
Maswa	2,004	1,761	1,860
Meatu (Mwanhuzi)	2,011	1,768	1,867
<b>Singida</b>	1,933	1,690	1,790
Iramba	1,945	1,702	1,802
Manyoni	1,917	1,675	1,774
Ikungi	1,928	1,686	1,785
Mkalama (Nduguti)	1,957	1,715	1,814
<b>Tabora</b>	1,996	1,754	1,853
Igunga	1,950	1,708	1,807

Kaliua	2,014	1,772	1,871
Ulyankulu	2,008	1,766	1,865
Nzega	1,961	1,718	1,817
Sikonge	2,008	1,765	1,865
Urambo	2,009	1,767	1,866
<b>Tanga</b>	1,825	1,586	1,745
Handeni	1,846	1,607	1,725
Kilindi	1,861	1,622	1,759
Korogwe	1,838	1,598	1,738
Lushoto	1,847	1,608	1,748
Mkinga (Maramba)	1,832	1,593	1,759
Muheza	1,830	1,591	1,745
Pangani	1,832	1,593	1,752

**B: BEI ZA JUMLA**

<b>Bei za Jumla - DSM</b>	<b>Petroli (Sh/L)</b>	<b>Dizeli (Sh/L)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Sh/L)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>1,737.38</b>	<b>1,494.85</b>	<b>1,594.04</b>

<b>Bei za Jumla - TANGA</b>	<b>Petroli (Sh/L)</b>	<b>Dizeli (Sh/L)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>1,720.47</b>	<b>1,481.29</b>

**Felix Ngamlagosi**  
**MKURUGENZI MKUU**  
**EWURA**